

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA**  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

Simu na. (025) 2520121

2520109, 2520035

Fax Na. (025) 2520117

baruapepe:ded.chunya@mbeya.go.tz

**Unapojibutafadhalitaja:**

Kumb. Na. CDC/VY/L.60/32/.....



S.L.P. 73,  
CHUNYA

Tarehe: 5/2/2018

AFISA UGANI(KILIMO/MIFUGO)

KATA/KIJIJI ZOTE

**CHUNYA.**

**YAH: CHANJO YA HOMA YA MAPAFU YA NG'OMBE (CBPP) AWAMU YA PILI**

Kichwa cha barua chahusika. Narejea Sheria ya Udhhibiti wa Magonjwa ya Mifugo (The animal disease Act 2003, No. 17) pamoja na maagizo ya Kamati za Kudumu za Halmashauri( Kamati ya Fedha na Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira) kuhusu udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo hasa **Homa ya Mapafu ya ng'ombe** kwa njia ya Chanjo.

Napenda kukutaarifu kuwa baada ya awamu ya kwanza ya Udhhibiti wa Ugonjwa wa Mapafu ya Ng'ombe (CBPP) kukamilika 2017, **Awamu ya Pili** ya chanjo itanza 1/3/2018 kama ratiba iliyoambatanishwa inavyoonesha.

Unaagizwa kutoa taarifa kwa wafugaji ili wafanye maandalizi muhimu:

1. Maandalizi ya kibanio chembamba na kiwe kirefu (mita 15)
2. Wakati wa chanjo, kila mfugaji aje na risiti ya kuonesha kuwa mifugo yake ilipigwa chapa. **Idadi ya mifugo itakayoletwa ilingane na ile iliyopo kwenye risiti ya chapa na kwenye daftari la ufugaji. Asiwepo yoyote wa kuficha mifugo.** Mfugaji hatahudumiwa kama mifugo haitakuwa na chapa wala risiti ya chapa.

Gharama ya Chanjo itakuwa ileile ya awamu ya kwanza (Yaani Tshs.1000/= kwa ng'ombe) na cheti cha kuchanja mifugo kitatolewa.

Afisa ugani unaagizwa kutumia muda huu wa kabla ya chanjo kuwatembelea wafugaji na kuwaelimisha kuhusu chanjo. Ni wajibu wa kila mfugaji kupeleka mifugo yake yote katika kituo cha chanjo na kugharamia chanjo hiyo. Ng'ombe watakochanjwa ni wale wenye umri wa

kuanzia miezi 6 na kuendelea ( Mifugo yote iliyopigwa chapa). Sheria zitatumika kwa atakayekaidi kuleta au atakayeficha mifugo kwa kuleta mifugo pungufu wakati wa kutekeleza agizo la chanjo.

Nakutakia maandalizi mazuri ya zoezi la chanjo.



Dkt. MATOGO, Benedict N.

DAKTARI WA MIFUGO

CHUNYA.

**DISTRICT VETERINARY OFFICES  
CHUNYA**